BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Tatu – Tarehe 29 Novemba, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wakala wa Barabara (ZANROAD) kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wakala wa Barabara (ZANROAD) kwa mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

93. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Ni sheria na kanuni zipi zinazowahusu Jeshi la Polisi kuwajibika katika kuchukua hatua stahiki dhidi ya wale wote wanaohusika katika kuharibu mila, silka, desturi na ustawi mwema wa tamaduni zetu.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

97. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kurundikana kwa taka katika maeneo mengi ya Jiji la Zanzibar bado ni changamoto inayopelekea uharibifu wa mazingira.

(a) Kwa vile utaratibu wa kukusanya taka na wananchi kulipia kwa kila mwezi unaonekana kukabiliwa na changamoto za kukaa taka kwa muda mrefu bila ya kuchukuliwa, ni sababu gani zinazopelekea hali hii.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuuendeleza utaratibu wa kukusanya taka na wananchi kulipia kwa mwezi kwa yale maeneo ambayo bado hayajafikiwa na utaratibu huu ikiwemo Jumbi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

3. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali iliahidi kufanya baadhi ya miradi kwa kutumia Mfumo wa "Engineering Procurement and Construction + Finance" (EPC+F).

Je, hadi hivi sasa ni miradi mingapi na yenye thamani ya kiasi gani imetekelezwa kupitia Mfumo huo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

45. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na mambo mengine, mtaala mpya unajikita katika kutengeneza umahiri.

(a) Ni aina gani za umahiri tunatarajia kuzitengeneza kwa wanafunzi wetu.

(b) Ni changamoto gani mpaka sasa Wizara yako inazipitia katika muendelezo wa kuutekeleza kwa vitendo mtaala mpya.

46. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tathmini inaonesha kwamba takribani wanafunzi wengi wa awali wanachelewa kujua kusoma na kuandika.

(a) Hali iko vipi kwa sasa.

(b) Ni changamoto gani hasa zinapelekea tatizo hili.

(c) Ni ipi mikakati ya Wizara ya kupambana na changamoto hii.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

33. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Kuna tafiti ngapi ambazo tathmini zake zinachanganua juu ya uharibifu wa utamaduni wetu.

(b) Ni zipi kati ya tafiti hizo zimetoa ufumbuzi wa majawabu muwala na miongozo mema.

79. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Miongoni mwa changamoto zinazorudisha nyuma maendeleo ya michezo kwa watu wenye ulemavu, ni pamoja na ukosefu wa mafunzo kwa walimu wa kufundisha watu wenye ulemavu, viwanja na vifaa wezeshi.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha changamoto hizo zinatatuliwa.

(b) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya kuendeleza michezo kwa watu wenye ulemavu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

74. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi,

Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi za kuyafungua Maeneo Huru ya Kiuchumi (Special Economic Zones) kama vile eneo huru maalum la Micheweni kwa ajili ya uwekezaji. Pamoja na juhudi kubwa za Serikali katika kulifungua eneo hilo, ipo changamoto kubwa ya eneo hili kukosa bandari (sea port) itakayokuwa na uwezo wa kurahisisha shughuli za uwekezaji.

(a) Je, bandari mpya ya Shumba itaweza vipi kuboresha shughuli za eneo hili huru la kiuchumi la Micheweni.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kufanya tathmini ya kina juu ya uwezekano wa bandari ya Shumba kuwa na uwezo wa kupokea meli kubwa za mizigo ili kusaidia eneo hili la uwekezaji.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na muda mrefu wa kuimarisha miundombinu ya usafirishaji katika eneo hilo huru la kiuchumi.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

27. MHESHIMWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

(a) Tafiti ngapi na zipi mpaka sasa zimefanyika katika kutoa muelekeo mzima wa upotevu wa mali zisizorejesheka ikiwa ni pamoja na mchanga, vifusi na mawe.

(b) Ni upi mpango mbadala wa Serikali kutokana na mashimo pamoja na mahandaki yanayoachwa baada ya uchimbaji wa mali zisizorejesheka kukamilika.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

14. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Tathmini ipo vipi juu ya miti ya matunda kutumika katika shughuli za mbao kwa ajili ya kutengenezea samani.

(b) Je, uko vipi muelekeo wa miaka 10 inayokuja mbeleni, iwapo hali hii haitadhibitiwa ipasavyo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

57. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Kivipi na kwa namna gani tukio la kihistoria la kufukiwa kwa bahari eneo zima la Darajani na Mji Mkongwe lilifanyika kwa faida ya wananchi.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Taarifa ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wakala wa Barabara (ZANROAD) kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**29 Novemba, 2024.** **KATIBU WA BARAZA.**